

## UGONJWA WA MIDOMO NA MIGUU (UMM)-FOOT AND MOUTH DISEASE

**Na Augustino Chengula**

UMM ni ugonjwa wenye maambukizi makubwa unaowapata ng'ombe, nguruwe, kondoo, mbuzi na nyati na ni ugonjwa mgumu sana kukabiliana nao. Kwa ujumla ni ugonjwa unawapata wanyama wote wenye kwato mbili wa kufugwa na wanyama pori. Dalili kubwa za ugonjwa huu ni homa, malengelenge (vesicles) mdomoni na puani, chuchu, kwato/nyayo, na vifo kwa wanyama wadogo.

UMM upo mashariki ya kati, Afrika (isipokuwa Afrika Kusini, Botswana, Namibia na Zimbabwe) na Amerika Kusini (isipokuwa Chile, Argentina Kusini, Uruguay, Guyana, Surinam na French Guiana). Mabara la Ulaya, Australia na Asia hayana ugonjwa huu isipokuwa kwa Asia upo Japani, Indonesia, na Korea. Kwa ujumla kwa Afrika ugonjwa huu unapatikana Jangwa la Sahara ya chini na juhudi za kuutokomeza bado hazijaoonyesha mafanikio. Na hii imesababishwa na ulewa mdogo wa aina ya virusi walioopo kwenye nchi husika.

**Madhara** –Ugonjwa huu unasababisha upotevu mkubwa wa kiuchumi kwa sababu ya vifo vya wanyama wadogo, kupungua kwa uzalishaji (maziwa, nguvu kazi, na kuzaliana) na kuzuiwa kwa biashara ya nyama na mazao mifugo ya ndani na kimataifa.

### **Kisababishi cha ugonjwa**

UMM unasababishwa na kirusi aitwaye *Aphthovirus* kilicho kwenye familia ya picornaviridae. Zipo aina saba za kirusi kinacho sababisa ugonjwa huu; A, O, C, Asia 1, SAT1, 2 & 3. Kwa Tanzania ni aina ya SAT 1, SAT 2 na O ndizo ambazo zimwekwisha kugunduliwa hadi sasa. Juhudi bado zinaendelea kufanyika na

wataamu kutoka SUA na wizara ya mifugo ili kubaini aina zilizopo  
zitaakazoweza utengenezaji wa chanjo ya kuzibiti virusi tulionao.

### **Uenezwaji**

Kwa kawaida ugonjwa huu huenezwa kwa njia ya kugusana kati ya mnyama mwenye ugonjwa huo na asiye nao. Lakini pia kwa njia ya hewa na kwa njia ya chakula. Wanyama wenye ugonjwa huu huwa na virusi vingi kwenye mfumo wa upumuaji hivyo hewa wanayo pumua huwa na virusi .Hata katika maji maji ya sehemu yoyote ile ikiwemo maziwa huwa na virusi hivi na hivyo ndama wana weza kupata ugonjwa kupitia maziwa ya mama wagonjwa.

Wanyama kama nguruwe wanaweza kupata ugonjwa kwa kula nyama, mizoga au maziwa toka kwa wanyama wenye ugonjwa.

Wanyama waliokwisha upata na kupona pamoja na wale walio chanjwa na chanjo hai wanaendelea kubeba virusi kwenye maeneo ya viriba hewa hadi miaka miwili na nusu, na miezi tisa kwa kondoo. Hii ni hatari kwani wataendelea kusambaza virusi bila wao kuonyesha dalili.

### **Dalili za UMM**

-Ugonjwa huanza kujitokeza kuanzia siku 2-14 tangu maambukizi kutegemea na uwingi wa virusi, aina ya mnyama na kirusi chenyewe.

-Dalili hujitokeza zaidi kwa ng'ombe wa maziwa na nguruwe wanao fungwa kwa wingi kuliko kwa kondoo na mbuzi.

-Homa ya nyuzi joto hadi 41 hujitokeza

-Kutoka ute/mate mdomoni

-Kukita miguu chini kadri malengelenge yanapo jitengeneza kwenye ulimi, fizi za meno, midomo, mguu, chuchu na kiwele hasa kwa wanao nyonyesha. Hii ni ishara ya maumivu wanayoyapata kutokana na vidonda.

-Wanyama wadogo waweza kufa kabla ya kuonyesha dalili yeyote ya uwepo wa malengelenge

-Utoaji wa maziwa hushuka, afya hudhoofu na ukuaji hupungua hata baada ya kupona

-Nguruwe hupoteza kwato zote za miguu wakati ng'ombe anaweza kupoteza moja au zote mbili za mguu.

-Viuvimbe vyenye malengelenge mdomoni hupotea ndani ya siku 7, japo ulimi waweza chukua siku zaidi.

-Vidonda vya kwenye kiwele vinaweza kupelekea ugonjwa wa kiwele (mastitis).

### **Utambuzi**

Mara nyingi dalili za ugonjwa hutosha kumuwezesha mfugaji kuutambua ugonjwa huu. Kwenye maabara ELISA na PCR hutumika kuutambua ugonjwa huu.

### **Matibabu**

Kama yalivyo magonjwa mengine ya virusi, ugonjwa huu hauna tiba maalumu.

Wanyama wenye vidonda husafishwa na kupakwa au kupuliziwa dawa ya kuzuia wadudu (antibiotics) na iodine. Dawa ya kuchoma (antibiotics) pia hutumika kupunguza maambukizi mengine ya magonjwa. Maeneo mengine majivu yameonyesha ufanisi katika usafishaji wa vidonda hasa mdomoni.

## **Kinga na jinsi ya kukabiliana na UMM**

Kinga kubwa ya UMM ni chanjo, japo changamoto ni kupata chanzo nzuri inayoendana na aina ya virusi waliopo kwenye eneo husika. Kukiwa na mlipuko wa ugonjwa eneo fulani ng'ombe wazuiwe kwenda eneo lisilo na ugonjwa.

Nchi zilizo fanikiwa kuondoa ugonjwa huu wana sera ya kuchinja ng'ombe wote wenye ugonjwa na mizoga huchomwa au kuzikwa na maeneo kusafishwa viruri na kupuliziwa dawa.